

## TAARIFA YA TATHMINI YA MAFANIKIO YA VIJANA WABUNIFU WALIOSHIRIKI KATIKA MAONESHO YA WIKI YA VIJANA TAREHE 8 - 14 AGOSTI 2016, BARIADI SIMIYU

### 1.0. UTANGULIZI

Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliratibu mchakato wa kuwapata vijana Wabunifu ili kushiriki na kuonesha kazi zao katika Maadhisho ya Wiki ya Vijana Kitaifa yaliyofanyika Mkoani Simiyu tarehe 8-14 Agosti 2016. Katika mchakato huo uliochukua vijana zaidi ya 30, walipatikana Vijana 10 ambao wamefanya ubunifu katika maeneo tofauti, ambayo ni habari na mawasiliano, afya, kilimo, viwanda vidogovidogo, ufugaji na nishati. Vijana hao walishiriki Maadhisho ya Wiki ya Vijana 2016, na kuonesha kazi zao kwa ustadi mkubwa uliowavutia watu wengi akiwemo aliyekuwa Mgeni Rasmi, Rais wa Zanzibar, Mh. Dr. Ali Mohamed Shein. Vijana Waabunifu hao ni pamoja na

- **Antony Nyagilo** - Mbunifu wa Programu na Katuni za kufundishia watoto na Vijana.
- **Deogras Mkawe** - Mbunifu wa kifaa cha teknolojia ya kuzuia ajali zinayosababishwa na Spidi kubwa ya mabasi.
- **Jeniffer Shigoli** - Mbunifu wa taulo za Wanawake(Sanitary pads) ambazo zinaweza kufuliwa na kutumiwa zaidi ya mara moja.
- **Dan Rwihiula** - Mfugaji wa Mende kibiashara kwa lengo maalum la upatikanaji wa chakula kizuri na cha bei nafuu kwaajili ya mifugo.
- **Hindoo Yusuph** - Mbunifu wa Mashine ya kukausha Matunda na Mbogamboga
- **Paul Kaparata** - Mbunifu wa Vitu mbalimbali kwenye sekta ya Kilimo hai(Organic Farming) kama drip za umwagiliaji, Kwa kutumia mabomba chakavu
- **Faisal Sultan** - Mbunifu wa kisima kinachotumia nishati ya jua kupandisha maji pamoja na boti ya umeme.
- **Kulwa Lusana** - Ni mlemau wa Ngozi(Albino) aliyekatwa mkono mmoja lakini anabuni na kufuma aina mbalimbali ya masweta kwa kutumia mkono mmoja.
- **Calvin Ndutwa** - Mbunifu wa Majiko ya Kupikia yanayotumia Nishati ya jua (Solar).
- **Peter Isare** - Mbunifu wa mfumo wa kielektroniki wa masoko ya kuuza mazao ya nafaka.

### 2.0. MAFANIKIO WALIYOPATA

Baada ya Maadhisho ya Wiki ya Vijana 2016, Ofisi ya Waziri Mkuu ilikaa kikao na vijana wabunifu walioshiriki maadhisho hayo, ili kubaini maeneo ya kuwasaidia ili kuendeleza kazi zao, ambapo baada ya kikao hicho, walitambulishwa kwa barua, kila mmoja kwenye Wizara husika. Yafuatayo ni baadhi ya mafanikio waliyopata baada ya Maadhisho ya Wiki ya Vijana 2017;

- 2.1. Kuanzisha taasisi yao ambayo imesajiliwa kisheria, ijulikanayo kama Tanzania Youth Innovation team (TAYOIT), amabayo wanafanya kazi kwa pamoja, kwa kushirikina na kupeana mawazo.

- 2.2. Kupata mirejesho chanya kutoka Wizara zilizoandikiwa barua, ambapo wamekubali kuwaendeleza na wengine wameunganishwa na taasisi mbalimbali za Wizara hizo.
- 2.3. Kuwezeshwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, kupata Mikopo kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.
- 2.4. Kufungua na kuboresha Viwanda vikubwa na vidogovidogo, ambavyo ni,
  - Joint Professional co.ltd Kinachojishughulisha na utengenezaji wa bidhaa za Asili, kama viungo nya chai, dawa ya Mbu na Biskuti.
  - Malkia Investment Company, inayojishughulisha na utengenezaji wa "reusable sanitary pads"
  - JATU Milling Company, Kiwanda cha kuzalisha unga na mchele
  - BRANDOS, Kiwanda (kampuni) ya kilimo na ukaushaji mbogamboga na matunda.
- 2.5. Kushiriki maonesho ya Kitaifa na Kimataifa kama vile SABASABA na NANENANE 2017, kuitia taasisi yao ya TAYOIT.
- 2.6. Mbunifu Jeniffer Shigoli alipata tuzo ya Mjasiriamali bora Afrika, katika kipengele cha elimu ya mazingira, Cassablanca Morocco Mwaka 2016.

### **3.0. CHANGAMOTO**

Pamoja na mafanikio makubwa waliyopata wabunifu hao, zipo changamoto mbalimbali ambazo bado zinawakabili,

- 3.1. Mitaji kwa ajili ya kukuza na kuongeza uzalishaji wa bidhaa zao
- 3.2. Maeneo/Ardhi ya kujenga viwanda na uzalishaji wa malighafi
- 3.3. Mashine na vifaa mbalimbali kwa ajili ya uzalishaji
- 3.4. Taratibu za kusajili makampuni na bidhaa zao kwenye mamlaka husika kuchukua muda mrefu
- 3.5. Magari kwa ajili ya kusambazia bidhaa zao

### **4.0. MAPENDEKEZO KWA OFISI YA WAZIRI MKUU**

- 4.1. Ofisi ya Waziri Mkuu, iwavezeshe kupata fursa ya mikopo kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ili kupata mitaji zaidi na kununua mashine, vifaa na magari ya kusambazia bidhaa zao.
- 4.2. Ofisi ya Waziri Mkuu, iwaalike kushiriki Maadhimisho ya Wiki ya Vijana 2017, kuitia taasisi yao ya "TAYOIT".
- 4.3. Ofisi ya Waziri Mkuu, iwaunganishe wabunifu hawa na Mamlaka za Mikoa na Halmashauri ili ziweze kuwapatia maeneo ya viwanda kulingana na Agizo la Serikali la kutenga maeneo kwa ajili ya vijana.
- 4.4. Ofisi ya Waziri iwaandikie barua za utambulisho "recommendation letter" ili kurahisha usajili wa Viwanda, Kampuni na bidhaa zao katika mamlaka husika ikiwemo TBS.